JARIDA LA MTANDAONI

# BURUJI NEWS

WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA

BURUJI NEWS | TOLEO NAMBA 001 | JULAI, 2021 | www.modans.go.tz

# Tanzania na Msumbiji Zaimarisha Ushirikiano



**Ndani:-** Waziri Kwandikwa amtembelea Jenerali "CHAKAZA"

Serikali yaahidi kuboresha Maslahi kwa Wafanyakazi

# Karibu
# MSANGANI MAKUTI CLUB

**Ni ukumbi wa kamandi ya Jeshi la Nchi Kavu**

*Upo Kilomita Sita kutoka barabara kuu iendayo Morogoro*

**Utapata huduma nzuri ikiwemo**

- *Vyakula vya aina mbalimbali,*
- *Vinywaji vya aina zote,*
- *Ukumbi kwa ajili ya sherehe,*
- *Eneo la kupaki magari na ulinzi wa kutosha*

**BEI NAFUU**



**KWA MAWASILIANO:**

**0767-276 203**





# PICHA YA JARIDA




## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**Jarida hili hutolewa na Ofisi ya Katibu Mkuu Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Kitengo cha Mawasiliano Serikalini. S.L.P. 2924 Dodoma, Tanzania/+255 (26) 2350762/ Nukushi:+255 (26) 23515225**

## WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA

**Yaliyoandikwa kwenye Jarida hili ni Mawazo ya Wandishi wetu, hayakusudii kuwasilisha sera, mtazamo wala maoni ya Uongozi wa Wizara**

## BODI YA UHARIRI

**MHARIRI MKUU**

Luteni Kanali Josephat Musira

**Naibu Mhariri Mkuu**

Kapten Mohamed Iddi

**Wahariri Habari**

Kapteni Mohamed Iddi
Sajini Lazarus Masanja

**Wandishi wa Habari**

Kapteni Mohamed Iddi

Sajinitaji Subira Asukile

Sajini Lazarus Masanja

Sajini Peter Lusse

**Wapiga Picha**

Kapteni Mohamed Iddi

Sajinitaji Subira Asukile

Sajini Lazarus Masanja

Sajini Peter Lusse

**Tovuti na Mitandao ya Kijamii**

Kapteni Mohamed Iddi

Sajini Lazarus Masanja

Sajini Peter Lusse

**Youtube - Ulinzi Channel**

Sajinitaji Subira Asukile
Sajini Peter Lusse

**Graphics & Design**

Sajini Lazarus Masanja

## YALIYOMO

Tanzania na Msumbiji Zaimarisha Ushirikiano................................5

Serikali yaahidi kuboresha Maslahi ya Wafanyakazi nchini...............6

Kwandikwa Ainisha Vipaumbe vya Wizara ya Ulinzi na JKT...........7

Wanawake Waadhimisha siku yao kwa Kishindo ............................9

Waziri Kwandikwa amtembelea Jenerali "CHAKAZA"....................10

Wazairi Kwandikwa atimiza ahadi ya kuwatembelea Wakuu wa Majeshi wastaafu...........................................................................11

Rais Samia atunuku Kamisheni kwa maafisa wapya....................13

Habari katika Picha.............................................................14 –15

Malenga wetu ............................................................................16

'Katumieni Weledi mlioupata Chuoni' Waziri Kwandikwa............18

Mjue Rais mwenye Umri Mdogo..................................................19

Misingi ya Upigaji Picha na Matumizi yake...................................20

Mahafali ya Tisa Chuo cha Taifa cha Ulinzi...................................21

# MAONI YA MHARIRI

Ndugu msomaji na mpenzi wetu tunapenda kukukaribisha katika Toleo letu la kwanza la Jarida Mtandaoni lijulikanalo kwa jina la ***'BURUJI NEWS*'"** linalotayarishwa na kuhaririwa na kuchapishwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini cha Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Kuanzishwa kwa Jarida hili kunafungua ukurasa mpya wa kuwapasha habari watanzania hususani watumishi waliopo chini ya Wizara kujua nini kimefanyika na nini kinaendelea, lakini pia hata walioko nje ya Wizara yetu watapata wasaa wa kujua nini tunakifanya.

Kuanzishwa huku kwa Jarida hili pia kuna lengo la kupanua wigo kwa wasomaji na wasikilizaji wetu. Hapo awali walikuwa wakitufuatilia na kutusoma ama kupitia Tovuti yetu ya Wizara ***www.modans.go.tz*** pamoja na Runinga Mtandao ya ***'Ulinzi Channel'.***

Katika kukidhi kiu na haja za wasomaji wetu, Timu ya wahariri, Wandishi na wapiga picha tamejipanga vilivyo kuhakikisha tunawafikia kwa kuwahabarisha wote popote walipo kupitia Jarida hili linalotarajiwa kuchapishwa mara moja kwa mwezi, kwa habari zilizohaririwa na kufanyiwa upembuzi yakinifu na wa kina na Wahariri wetu wabobezi.

Jarida hili sehemu kubwa litakuwa katika mtandao na nakala chache zitachapwa na kusambazwa katika ofisi zetu za Wizara.

Ni matarajio yangu kuwa wasomaji na wasikilizaji wetu watatuunga mkono kwa kufuatilia na kusoma habari zetu zitakazokuwa zikichapishwa kupitia Jarida hili na kisha kutoa maoni na ushauri wenye lengo la kuboresha machapisho yatakayoendelea kuchapishwa.

***Kwa maoni na ushauri tafadhali wasiliana nasi kupitia;***

***gcumod@gmail.com,***

***info@modans.go.tz***

**DIRA YA WIZARA:**

Kuwa Taasisi iliyotukuka ya kulinda na kudumisha amani na usalama wa Taifa letu.

**DHIMA YA WIZARA:**

Kuendelea kulinda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania dhidi ya adui wa aina yoyote kutoka ndani na nje ya nchi kwa kuhakikisha kuwa mamlaka na maslahi mapana ya nchi yetu yanakuwa salama.

# JE WAJUA?

## HISTORIA YA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA

Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni miongoni mwa Wizara kongwe zenye historia ndefu iliyosheheni mafanikio makubwa, Wizara hii ilianza rasmi mara baada ya Uhuru mwaka 1961 huku ikijulikana kwa jina la **WIZARA YA MAMBO YA NJE NA ULINZI**.

- Mwaka 1964 Wizara hii ilibadilishwa jina na kuitwa **WIZARA YA ULINZI JKT NA VIJANA** na kuhamishwa kwenda **Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais**.
- Mwaka 1972 Wizara hii iliondolewa **Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais** na kuwa Wizara inayojitegemea na kuitwa **WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA**.
- Mwaka 1989 Wizara hii ilifanyiwa mabadiliko mengine kwa kuhamishiwa **Ofisi ya Rais** huku ikiendelea kuitwa **WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** na hivyo kupelekea Waziri wake atamkwe kama **WAZIRI WA NCHI KATIKA OFISI YA RAIS ANAYESHUGHULIKIA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA.**
- Mwaka 1995 Wizara hii ilifanyiwa mabadiliko tena kwa kuondolewa katika Ofisi ya Rais na kuwa **WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** hali inayoendelea hadi sasa.

Katika Kipindi chote hiki Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa mambo mengi na yenye mafanikio makubwa huku ikiongozwa na Mawaziri 16 kwa nyakati tofauti, Manaibu Waziri 2 na Makatibu Wakuu Wakuu 19 Manaibu Katibu Wakuu 4.

Kwasasa Uongozi uliopo madarakani katika Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni Waziri ni Mheshimiwa CPA Elias John Kwandikwa (Mb) na Katibu Mkuu ni Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe

# Tanzania na Msumbiji Zaimarisha Ushirikiano



***Waziri wa Ulinzi na JKT, Mheshimiwa Elias John Kwandikwa (Mb) wakipongezana na Waziri wa Ulinzi wa Msumbiji, Mheshimiwa Jaime Augusto Bessa Neto siku ya kufunga Mkutano wa Tatu wa Tume ya Kudumu ya Pamoja baina ya Tanzania na Msumbiji kuhusu Ulinzi na Usalama uliofanyika katika Ukumbi Julius Nyerere International Convention Centre (JNICC), Jijini Dar es Salaam.***

**Na Luteni Kanali Josephat Musira**

Mahusiano baina ya Tanzania na Msumbiji yameendelea kudumishwa katika nyanja mbalimbali za Ulinzi na Usalama katika kubadilishana maarifa, taarifa, mafunzo na mazoezi ya pamoja.

Hayo yamebainishwa wakati wa Mkutano wa Tatu cha Tume ya Kudumu ya Pamoja baina ya Tanzania na Msumbiji kuhusu Ulinzi na Usalama (The Joint Permanent Commission on Defence and Security – JPCDS), kilichofanyika katika Ukumbi Julius Nyerere International Convention Centre, Jijini Dar es Salaam kwa siku tatu mfululizo kuanzia tarehe 03 – 05 Juni, 2021.

Ujumbe wa Tanzania uliongozwa na Waziri wa Ulinzi na JKT, Mheshimiwa Elias John Kwandikwa (Mb), akiambatana na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Hamza Khamis Chillo (Mb), Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na JKT, Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe, Katibu Mkuu wa Wizara wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Bw. Christopher Kadio, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Venance Salvatory Mabeyo, Wakuu wengine wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama pamoja na Taasisi za Serikali.

Kwa upande wa Msumbiji ujumbe huo uliongozwa na Waziri wa Ulinzi wa Msumbiji, Mheshimiwa Jaime Augusto Bessa Neto, akiambatana na Waziri wa Mambo ya Ndani Mheshimiwa Amade Miquidade, Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi wa Taifa, Bw. Casimiro Augusto Mueio na viongozi wengine kutoka Taasisi za Ulinzi na Usalama.

Mkutano huo ulipokea na kujadili ripoti mbalimbali zilizowasilishwa kutoka Kamati zake tatu yaani Ulinzi (Defence Committee), usalama wa raia (Public Security Committee) pamoja na ile ya usalama wa Taifa (State Security Committee) na hatimaye kupitisha maazimio yaliyohusu mafunzo na mazoezi ya pamoja baina ya majeshi ya nchi mbili hizi, kuongeza shughuli za doria za mpakani, kuimarisha ulinzi wa mpaka na kuanzisha chombo maalum kitakachosaidia kupambana na uhalifu baina ya mataifa haya.

Aidha, Tume hiyo ililaani vikali mashambulizi ya kigaidi yaliyofanywa katika jimbo la Cabo Delgado nchini Msumbiji, ambapo watu kadhaa walipoteza maisha, wengine kukimbia makazi yao pamoja na uharibifu wa mali za umma na binafsi. Kwa kufanya hivyo, pande mbili hizi zimekubaliana kushirikiana katika mapambano dhidi ya kikundi hiki cha kigaidi kwa kubadilishana taarifa, maarifa pamoja na mambo mengine mengi.

Hii ni mara ya pili kwa mkutano kama huo kufanyika nchini Tanzania, Mkutano wa kwanza ulifanyika Dar es Salaam, Tanzania tarehe 04 - 06 Februari, 2011 ambapo Tume hii ilianzishwa rasmi. Na mkutano wa pili ulifanyika Maputo Msumbiji tarehe 02 – 04 Aprili, 2013 na mkutano ujao unatarajiwa kufanyika mwakani nchini Msumbiji mwezi Juni kwa tarehe na mahali itakayopangwa hapo baadaye.

# Serikali yaahidi kuboresha Maslahi ya Wafanyakazi nchini



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Hassan Suluhu akihutubia Wafanyakazi siku ya Maadhimisho ya Sherehe za Mei Mosi Kitaifa katika uwanja wa CCM Kirumba Jijini Mwanza.*

**Na Sajini Lazarus Masanja**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeahidi kuendelea kutatua kero na Changamoto zinazowakabili Wafanyakazi na kuwafanya waweze kufanya kazi zao za kila siku kwa ufanisi.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan alivyasema hayo katika Uwanja wa CCM Kirumba alipokuwa akiwahutubia Maelfu ya Wafanyakazi katika siku ya Maadhimisho ya Wafanyakazi Duniani iliyofanyika Kitaifa Jijini Mwanza.

"Serikali imeanza kuzitafutia ufumbuzi baadhi ya Changamoto zinazowakabili Wafanyakazi nchini ikiwemo Bima ya Afya ambapo kwa sasa ipo katika mchakato wa kuanzisha Bima ya Afya kwa Wafanyakazi wote" Alisema Rais Samia.

Aidha, Sereikali imesikia kilio cha Wafanyakazi kuhusu ukomo wa Umri wa Tegemezi kwa ambapo kwa upande wa Bima ya Afya imeongeza Umri wa tegemezi kutoka miaka 18 hadi miaka 21.

Changamoto nyingine aliyoizungumzia Mhe Rais ni makato ya Bodi ya Mikopo ambapo alisisitiza kuwa Serikali imeamua kubakia na asilimia 15 anayokatwa mdaiwa kwenye mshahara wake na Serikali imefuta asilimia 6 iliyokuwa inakatwa kama adhabu kwa mdaiwa. Mhe. Rais Samia pia amewasihi wanufaika wa mikopo hiyo kuendelea kulipa mad

Kuhusu kupandisha Mshahara Mhe. Rais alisema "Mishahara haijaongezwa kwa muda mrefu kwa sababu mbalimbali ikiwemo janga la ugonjwa wa Corona lakini nawaahidi mwakani tarehe kama ya leo nitapandisha Mishahara"

Mhe. Samia alisema Serikali katika mwaka mpya wa Fedha itapunguza Kodi na kufuta tozo mbalimbali kwa wafanyakazi.

"Tunakwenda kuboresha maslahi kwenye mwaka ujao wa fedha ikiwemo kupandisha vyeo watumishi elfu 85mpaka elfu 91 ambao wataigharimu Serikali Shilingi Bilioni 449, kulipa malimbikizo Shilingi Bilioni 60, mabadiliko ya Kimuundo wa Utumishi yatakayoigharimu Serikali Shilingi Bilioni 120 na pia kuajiri watumishi wapya takribani elfu 40 katika Sekta ya Afya na Elimu, ajira hizi mpya zitaigharimu Serikali Shilingi Bilioni 239".

Akihitimisha Hotuba yake Mhe. Rais Samia alisema Jitihada hizi na nyinginezo zitasaidia kuwapunguzia Wafanyakazi ugumu wa Maisha.




*Sehemu ya Wafanyakazi wa Wizara mbalimbali wakiwemo wa Wizara ya Ulinzi na JKT wakipita mbele ya mgeni Rasmi Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Hassan Suluhu siku ya Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi) iliyofanyika katika Uwanja wa CCM Kirumba Mwanza.*

# Waziri Kwandikwa Ainisha Vipaumbe vya Wizara ya Ulinzi na JKT

## ● Alipokuwa akiwasilisha Bajeti ya Wizara Bungeni



*Waziri wa Ulinzi na JKT, Mheshimiwa Elias John Kwandikwa (Mb) akiwasilisha Madirio ya Mapato na Matuzi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.*

**Na Luteni Kanali Josephat Musira**

Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Elias John Kwandikwa (mb), ameainisha vipaumbele vya wizara yake kwa Mwaka wa Fedha ujao wa 2021/2022.

Mheshimiwa Kwandikwa ameyasema hayo alipokuwa akiwasilisha Bungeni Hotuba ya Bajeti ya Wizara yake kwa Mwaka Fedha 2021/2022 tarehe 21 Mei, 2021 ambapo pamoja na mambo mengine amesema, Mpango wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 ni kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na ufasaha kulingana na Dira na Dhima ya Wizara.


Mheshimiwa Waziri amesema Mwelekeo wa shughuli zinazokusudiwa kufanyika katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 utazingatia maeneo ya kipaumbele yakiwemo: Kuliimarisha Jeshi kwa kulipatia zana na vifaa vya kisasa, mawasiliano, rasilimali watu pamoja na kutoa mafunzo; Kuendelea za jitihada za utatuzi wa changamoto za mipaka ya nchi yetu na nchi jirani; Kuboresha mazingira ya kazi, makazi na kuimarisha upatikanaji wa huduma stahiki na Kuendelea kujenga uwezo wa Jeshi la Kujenga Taifa kwa zana na vifaa vya kilimo ili liweze kujitosheleza kwa chakula na kuboresha miundombinu katika vikosi ili liweze kuchukua vijana wengi zaidi.

Maeneo mengine aliyoyainisha ni pamoja na Kuendeleza tafiti na uhawilishaji wa teknolojia kwa ajili ya kuzalisha bidhaa na huduma kwa matumizi ya kijeshi na kiraia; Kuimarisha na kuratibu Mafunzo ya Jeshi la Akiba; Kuimarisha ushirikiano na Jumuiya za Kimataifa, Kikanda na nchi moja moja katika nyanja za kijeshi na kiulinzi; Kuendelea kushirikiana na Mamlaka za Kiraia; na Kufanya upimaji, uthamini na ulipaji fidia ya ardhi katika maeneo yaliyotwaliwa kwa ajili ya matumizi ya jeshi.

Aidha, Kuhusu Dira na dhima ya Wizara ya Ulinzi na JKT, Mheshimiwa Kwandikwa amesema **Dira** ya Wizara ni kuendelea kuwa Taasisi iliyotukuka ya kulinda na kudumisha amani na usalama wa Taifa letu. Aidha, **Dhima** ya Wizara ni kuendelea kulinda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania dhidi ya adui wa aina yoyote kutoka ndani na nje ya nchi kwa kuhakikisha kuwa mamlaka na maslahi mapana ya nchi yetu yanakuwa salama.

Na mwisho, Mheshimiwa Waziri alimaliza kwa kubainisha kuwa, katika kufanikisha Dira na Dhima, Malengo ya Wizara yameendelea kuwa na Jeshi dogo lenye wataalamu, zana na vifaa vya kisasa; Kuendelea kuwapa Vijana wa Kitanzania ukakamavu, maadili mema, utaifa, moyo wa uzalendo na uwezo wa kujitegemea; Kujenga uwezo katika tafiti mbalimbali na uhawilishaji wa teknolojia kwa matumizi ya Kijeshi na Kiraia; Kuimarisha Jeshi la Akiba; Kusaidia Mamlaka za Kiraia; na Kudumisha amani na usalama kwa kushirikiana na nchi nyingine duniani.

# JITEGEMEE SECONDARY SCHOOL




**Tunatoa Elimu ya Sekondari kwa kidato cha kwanza hadi kidato cha nne, na kidato cha tano na sita kwa michepuo ya PCB, PCM, PGM, CBG, EGM, ECA, HGE, HGL, HGK na HKL**
**Pia Sekondari miaka miwili (QT)**

Tunafundisha kozi za kompyuta zinazoratibiwa na VETA.

* Basic Skills in ICT.
* ICT intirmediate cource.
* Applied Computerised Accounting.
* Introduction to Media in Education and Training.



**Mawasiliano:**
Mob: 225715169654 na 255713190324
Tovuti: www.jitegemee-sec.com Barua pepe: jitegsec@yahoo.com

# Wanawake waadhimisha siku yao kwa Kishindo

**Na Sajinitaji Subira Asukile**

Machi 8, 2021 ni Siku ya Wanawake Dunian ambapo Wanawake wa Mkoa wa Dodoma walijitokeza kwa wingi na kuungana na Wanawake wengine duniani kote kuadhimisha siku ya Wanawake duniani maadhimisho ambayo yalifanyika katika Wilaya ya Bahi Mkoani Dodoma.

Kila mwaka siku hii maalum ya wanawake duniani inakumbusha umuhimu wa mwanamke katika jamii, kwa mambo mengi yafanywa na mwanamke katika Nyanja mbalimbali hususani kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Sherehe hii kwa Mkoa wa Dodoma iliambatana na shamrashara ambazo zilifanyika katika Wilaya ya Bahi ambapo mgeni rasmi katika Maadhimisho hayo alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Bahi Bi.Mwanahamisi Munkunda ambapo Maadhimisho hayo yalichagizwa na Kauli Mbiu isemayo "***Wanawake katika Uongozi ni chachu ya kufikia Dunia yenye usawa"***.

Akitoa taarifa fupi ya wilaya ya Bahi katika siku hiyo ya wanawake duniani, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi Dkt. Fatuma Mganga alisema "Wanawake tunaweza na tuna nguvu na ndiyo mawaziri wakuu wa kaya zetu zote, hivyo kila mwanamke ajue kuwa yeye ni Kiongozi.

Amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali yake kwa kuwaamini wanawake katika maeneo mengi muhimu serikalini, kwa upande wa Elimu Wilaya ya Bahi ina wanafunzi 56 elfu kwa shule za Msingi 72, kati ya hao zaidi ya asilimia 55% ni watoto wa kike, hali hii inasisimua na inatuambia tunaenda kwenye mageuzi, katika Uongozi Kiongozi mkuu wa Serikali wa Wilaya ni mwanamke, Mkurugenzi mtendaji ni mwanamke na idara tatu zinaongozwa na wanawake ikiwemo idara ya manunuzi ni wanawake wanaofanya kazi vizuri kwa uaminifu,hivyo tunaheshimu tumepewa nafasi, Agenda yetu kubwa ni lazima kuonyesha wanawake tunaweza, na kwa mwaka huu Bahi imekuwa ya kwanza katika ufaulu wa watoto wa shule ya msingi Mkoani Dodoma.

Naye Mkuu wa Wilaya Bi. Mwanahamisi Munkunda ambaye ndie Mgeni rasmi amesema "Serikali inamkakati wa kuwawezesha wanawake kushiriki na kupewa madaraka makubwa na majukumu muhimu katika serikali ya awamu ya Sita kwa kuwa inawaamini wanawake, hivyo hatuna budi wanawake kufanya kazi kwa bidii na kuonyesha uwezo, maarifa na juhudi zetu kwa maslahi mapana ya Taifa letu, tusikubali kutumika kwa namna nyingine itakayotufanya kuonyesha udhaifu na kusababisha matokeo mabaya ya utendaji kazi".

Amepongeza Halmashauri ya Wilaya ya Bahi kwa utekelezaji wa mkakati wa serikali kuyawezesha makundi maalum ambayo ni wanawake, vijana na walemavu kwa mapato yake ya ndani kwa asilimia 10%, Bahi imeweza kutoa mikopo ya Sh. Milion 102.9 kwa vikundi 72 ambapo vikundi 56 ni wanawake, ambao wanaongoza kurejesha fedha hizo kwa kuwa wamekuwa vizuri kiuchumi na wanaendelea na ujasiliamali.

Sherehe hizo zilihudhuriwa pia na Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wanawake CCM-Taifa (UWT)Taifa, Mama Qeen Mulozi ambaye alisisitiza wanawake viongozi kuwashika mkono wanawake wengine walioko ngazi zote, Mkuu wa Wilaya Dodoma Mjini, viongozi wa Serikali, Viongozi wa Vyama, viongozi wa taasisi mbalimbali na wadau wengine wa wanawake Mkoa wa Dodoma wameshiriki maadhimisho hayo.




***Baadhi ya watumishi wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika picha ya pamoja siku ya maadhimisho ya Wanawake Duniani Kimkoa Wilayani Bahi Dodoma.***

# Waziri Kwandikwa amtembelea Jenerali 'CHAKAZA'



**David Bugozi Musuguri Jenerali (Mstaafu )**

**Na Kapteni Mohamed Idd**

Huwezi kumsimulia Jenerali mstaafu David Bugozi Musuguri bila kuelezea Vita ya Kagera, vita ambayo aliiongoza kupambana na Iddi Amin Dada na kumpa jina maarufu la Jenerali Chakaza.

Kwakutambua mchango wake mkubwa kwa Taifa hili hivi karibuni Waziri wa Ulinzi na JKT Mheshimiwa Elias John Kwandikwa (Mb) alifanya ziara ya kumtembelea Mkuu huyo wa Majeshi Mstaafu Jeneral David Bugozi Musuguri nyumbani kwake Butiana Mkoani Mara.

Katika ziara hii Waziri Kwandikwa alipata nafasi ya kumjulia hali kwa mara ya kwanza tangu alipoapishwa kuwa Waziri wa Ulinzi na JKT ambapo pamoja na mambo mengine alipata wasaa wa kuongea naye mambo mbalimbali na kubadilishana mawazo.

Katika ziara hii Waziri Kwandikwa alitumia wasaa huo kumkabidhi gari mpya aina ya Toyota Land Cruiser VXR kwa ajili ya Matumizi yake ya kila siku.

Akizungumza wakati wakati wa maongezi yao Waziri Kwandikwa Alisema "nimejiwekea utaratibu wa kuwatembelea Wastaafu hususani waliowahi kushika Wadhifa mkubwa Jeshini ambapo kwa kuanza nitatembelea Wakuu wa Majeshi wastaafu ili niweze kuwaona, kuwajulia hali na waweze kunipa historia ya wapi tulipotoka, kwani hawa ni watu muhimu ambao wamelipigania taifa na Jeshi hili na kulifanya kuwa Jeshi la mfano la kuigwa Barani Afrika na Duniani kote.

Wakati wa Vita ya Kagera iliyohusisha Majeshi ya Tanzania na Majeshi ya Nduli Iddi Amin Dada wa Uganda ambapo mwaka 1978 Iddi Amin alivamia Kagera na kushusha bendera ya Tanzania na kupandisha ya Uganda huku akiitangazia Dunia kuwa sehemu hiyo ni mali ya Uganda.

Hapa ndipo Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere akiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipotangaza Vita na Majeshi yetu ya Ulinzi yakiongozwa na Jenerali Musuguri kwa jina maarufu la Jenerali CHAKAZA.

Hakika Jenerali CHAKAZA alimchakaza Nduli Iddi Amin na kumfanya akimbilie Libya ambako aliishi mpaka alipofariki.

Jenerali Davidi Bugozi Musuguli alikuwa Mkuu wa Majeshi wa tatu wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania JWTZ kuanzia mwaka 1980-hadi 1988.

Hii ni ziara ya kwanza kuwatembelea waliowahi kuwa Wakuu wa Majeshi ya ulinzi kwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mheshimiwa Elias John Kwandikwa tangu iingie madarakani.



***Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga taifa Mheshimiwa Elias John Kwandikwa akiwa nyumbani kwa Jenerali Mstaafu Davidi Musuguli alipomtembelea nyumbani kwake kumjulia hali***

# Waziri Kwandikwa atimiza ahadi yake Kuwatembelea Wakuu wa Majeshi Wastafu



***Waziri wa Ulinzi na JKT Mhe. Elias Kwandikwa(Mb) kushoto akiwa nyumbani kwa Mkuu wa Majeshi (Mstaafu) Jenerali Davis Mwamunyange siku alipomtembelea .***

**Na Luteni Kanali Josephat Musira**

Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mhe. Elias John Kwandikwa (Mb) mwanzoni mwa Mwezi Julai alifanya ziara ya kuwatembelea Wakuu wa Majeshi wastaafu walioko Dar es Salaam kama alivyokuwa ameahidi hapo awali.

Wa kwanza kutembelewa na Mhe. Waziri alikuwa ni Jenerali Davis Adolf Mwamunyange; Akiwa nyumbani kwa Jenerali (Mstaafu) Mwamnyange katika Mitaa ya Kilongawima Jijini Dar es Salaam Mhe. Kwandikwa alisema ameamua kufanya ziara za kuwatembelea Wastaafu hawa ili kuwajulia hali na kwakutambua mchango wao mkubwa waliotoa kwa Jeshi letu tangu kuanzishwa kwake.

"Tangu kuanzishwa kwa Jeshi letu tumeendelea kupata mafanikio makubwa kutokana na mchango wenu wa kuwafundisha, kuwatayarisha na kuwasuka Wanajeshi wetu ambao wamekuwa wakifanya kazi nzuri" Alisema Waziri Kwandikwa.

Kwa upande wake Jenerali (Mstaafu) Adolf Mwamnyange alimpongeza Mhe. Waziri Kwandikwa kwa uamuzi wake wa kutenga muda wake kuwatembelea Wakuu wa Majeshi wastaafu kuwajulia hali kwani kwa kufanya hivyo ni heshima kubwa kwao.

"Ni heshima kwetu kutembelea na kutujulia hali, kwakweli tumepata faraja kubwa saana" Alisema Jenerali (Mstaafu) Mwamunyange

Wakati huo huo Mhe. Waziri Kwandikwa amemtembelea Jenerali (Mstaafu) Robert Philimon Mboma nyumbani kwake eneo la Tangi Bovu Jijini Dar es Salaam.

Akiwa nyumbani kwa Jenerali (Mstaafu) Robert Mboma Mhe. Kwandikwa alisema licha ya kustaafu Majenerali hawa bado ni sehemu ya familia ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa maana hiyo.

"Licha ya kustaafu bado ninyi ni sehemu ya familia yetu, tukiwatembelea tunapata fursa ya kufungua mawasiliano kwa lengo la kutatua changamoto zilizopo"Alisema Waziri Kwandikwa.Naye Jenerali (Mstaafu) Robert Mboma alisema viongozi wanapowatembelea nao wanapata fursa ya kuongea.

"Mkitutembelea nasi tunapata fursa ya kuongea na kushauri baadhi ya mambo ambayo ni muhimu kwa Taifa letu" Alisema Jenerali (Mstaafu) Mboma.

Ziara hii ya Mhe. Waziri ni muendelezo wa Ziara zake za kuwatembelea Wakuu wa Majeshi wastaafu ambapo ziara ya kwanza aliifanya Wilayani Butiama alipomtembelea Jenerali (Mstaafu) David Bugozi Musuguri na baadaye Jenerali (Mstaafu) Mirisho Samhagai Sarakikya.



***Waziri wa Ulinzi na JKT Mhe. Elias Kwandikwa akiwa na Mkuu wa Majeshi mstaafu Jenerali (Mstaafu) Robert Mbomba alipomtembelea nyumbani kwake TangiBovu Jijini Dar es Salaam.***

# SUMAJKT Catering & Recreation Services




**Kumbi zetu zina viyoyozi muda wote, zina vyumba vya VIP. ZInakodishwa kwa shughuli mbalimbali kama vile Harusi, Send Off, Mikutano, Kitchen Party nk.**

**Pia tunatoa huduma ya chakula katika sherehe mbalimbali.**

**Kwa mawasiliano:**

**Simu: 0753 242 363,0737 541 313, 0785 786 951**
**Email: sumajktcatering@sumajkt.co.tz**

# Rais Samia Atunuku Kamisheni kwa Maafisa Wapya





*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Hassan Suluhu akitunuku Kamisheni maafisa wapya katika Viwanja vya Ikulu Chamwino Jijini Dodoma, pembeni ni maafisa wapya wakila kiapo cha Utii kwa Amiri Jeshi Mkuu*

**Na Sajini Lazarus Masanja**

Ilikuwa Aprili 17 2021 ambapo Historia ya Tanzania iliandikwa baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kutunuku Kamisheni kwa Maafisa wapya katika viwanja vya Ikulu ya Chamwino Jijini Dodoma.

Sherehe hizo za Kamisheni zilifanyika kwa mara ya kwanza jijini Dodoma Makao Makuu ya nchi kabla ya hapo sherehe hizi zilikuwa zikifanyika chuoni – Monduli Mkoani Arusha kabla ya kuhamishiwa viwanja vya Ikulu - Dar es Salaam.

Kabla ya kutunuku Kamisheni, Mheshimiwa Samia alipokea salamu ya heshima kwa Rais na kisha kukagua gwaride lililoandaliwa na Chuo cha Maafisa- Monduli chini ya usimamizi wa Mkuu wa Chuo hicho, Brigedia Jenerali Jairos Jacob Mwaseba.

Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu ametunuku Kamisheni kwa mara ya kwanza tangu aapishwe rasmi tarehe 19 Machi, 2021 kuwa Rais wa Awamu ya Sita kufuatia kifo cha Rais wa Awamu ya Tano, Hayati John Pombe Joseph Magufuli kilichotokea tarehe 17 Machi, 2021 katika Hospitali ya Mzena jijini Dar es Salaam.

Rais amepewa madaraka ya kutunuku Kamisheni na ibara ya 148 (2)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Toleo la mwaka 1977 na kifungu cha 29 (5) ya Sheria ya Ulinzi wa Taifa ya mwaka 1966.

Akitoa taarifa fupi kwa Rais kuhusu mafunzo, Mkuu wa Chuo cha Maafisa, Brigedia Jenerali Jackson Jairos Mwaseba alisema Jumla ya wanafunzi wanaotarajia kupata kamisheni ni 386 kati yao 51 ni wanawake na wanaume 335 miongoni mwao wapo Maafisa wanafunzi 17 ambao wamepata mafunzo kutoka Nchi rafiki wakiwemo 1 kutoka Burundi, 2 kutoka China, 4 kutoka India, 5 kutoka Kenya, 1 kutoka Marekani, 2 kutoka Morocco,na 2 kutoka Ujerumani.

Pia kuna wahitimu waliopata mafunzo yao hapa Nchini kutoka Nchi rafiki wakiwemo 2 kutoka Falme za Eswatini na 5 kutoka Jamhuri ya Kenya. Mafunzo hayo yamefanywa kwa kushirikiana na Chuo cha Uhasibu Arusha ambacho kinaipa hadhi ya chuo cha Monduli kutoa Shahada kwa mwongozo wa TCU na NACTE. Mafunzo hayo yaligawanyika katika makundi makuu mawili; moja likiwa ni Kundi la 68 kozi ya Kawaida (Regular Course) mafunzo yaliyodumu kwa kipindi cha mwaka mmoja yaliyoanza mwaka 2020, Kundi la Pili ni wale wa Shahada ya Sayansi ya kijeshi (Bachelor of Military Science) 1/17 mafunzo yaliyodumu kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2

Jukumu la msingi la Chuo cha Maafisa wanafunzi Monduli ni kufundisha Maafisa wanafunzi (Officer Cadets) kwa weledi na viwango vinavyo hitajika kimataifa watakao kuwa tayari kulitumikia Jeshi na kulinda maslahi mapana ya nchi yetu.

Chuo ambacho kilianzishwa mwaka 1969 kama shule ya Maafisa wanafunzi Kurasini huko Dar es salaam ambacho kwa sasa ni Chuo Cha Maafisa wa polisi.

Kabla ya kuanzishwa kwake Maafisa wa Jeshi letu walikuwa wakipata mafunzo katika nchi mbalimbali zikiwemo Canada, Ethiopia, India, Israel, Misri, Pakistan, Sudan, Uingerza na Urusi. Kutokana na kukua kwa Jeshi na kuongezeka majukumu ya utendaji, umuhimu wa kuwaa na maafisa waliofunzwa kwa kufuata maadili ya Nchi yetu, kuliweka msukumo wa kuanzisha chuo cha Maafisa wanafunzi kilichozinduliwa rasmi tarehe 6 Februali 1969 na aliyekuwa Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Amiri jeshi mkuu Hayati Mwalimu Julias Kambarage Nyerere na kuhamishiwa MONDULI-ARUSHA Septemba 1976. Chuo cha Kijeshi-Monduli kinaendelea kudumisha kauli mbiu yake "DAIMA MBELE".

# HABARI KATIKA PICHA



*Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Frof. Ibrahim Hamis Juma akimuapisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan Ikulu Dar es Salaam.*



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akikagua gwaride maalumu katika viwanja vya Ikulu' Jijini Dar es Salaam muda mfupi baada ya kuapishwa.*



*Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama (NUU) Mhe. Mussa Azzan Zungu akiwa ameambatana na Kamati yake pamoja Waziri wa Ulinzi na JKT Mhe. Elias Kwandikwa (Mb) walipotembelea Chuo Cha Mafunzo ya Kijeshi - Monduli Jijini Arusha .*



*Katibu Mkuu Wizara ya Ulinzi na JKT Dkt. Faraji Mnyepe akielezea jambo wakati wa Mkutano wa Tatu wa Tume ya Kudumu ya Pamoja baina ya Tanzania na Msumbiji kuhusu Ulinzi na Usalama (The Joint Permanent Commission on Defence and Security Convention Centre – JPCDS), kilichofanyika katika Ukumbi wa Julius Nyerere Jijini Dar es Salaam.*



*Waziri wa Ulinzi na JKT Mhe. Elias Kwandikwa(Mb) akiwasili katika Mahafali ya 35/20 katika Chuo cha Ukamanda na Unadhimu (CSC) Duluti Jijini Arusha.*



*Waziri wa Ulinzi na JKT Mhe. Elias Kwandikwa(Mb) akisalimiana na Maafisa wa Vikosi vya Base ya Shinyanga alipofanya ziara Mkoani humo hivi karibuni*

# HABARI KATIKA PICHA



*Vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa (Service Girl) wakifanya usafi katika Kitalu cha Miche ya Michikichi katika Kikosi cha Bulombola Kigoma, pembeni ni kiongozi wao Sajini taji Mushi.*



*Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mhe. Elias Kwandikwa (Mb) akiwa na mgeni wake Mkuu wa Majeshi ya Rwanda Jenerali Jean Bosco Kazura (kulia) alipotembelea nchini kulia ni Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi nchini Jenerali Venance Mabeyo.*



*Waziri wa Ulinzi na JKT Mhe. Elias Kwandikwa(Mb) na Katibu Mkuu Wizara ya Ulinzi na JKT Dkt. Faraji Mnyepe katika picha ya pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi la Wizara hiyo Magadu Mess Morogoro.*



*Watumishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waliohudhuria mafunzo ya JKT katika Kikosi cha JKT-Makutupora hivi karibuni*



*Mkuu wa Utumishi Jeshini Meja Jenerali Paul Kisesa Simuli Akikagua Gwaride Rasmi Lililoandaliwa na Askari wapya Kundi Maalum 05/21 Wakati wa Kufunga Mafunzo hayo Katika Shule ya Mafunzo ya Awali ya Kijeshi RTS– Kihangaiko Mkoani Pwani.*



*Kamishna wa Sera na Mipango Wizara ya Ulinzi na JKT Bw. Obed Sayore akimkadhi zawadi Bi. Mariam Mwinjuma aliyekuwa akifanyia kazi katika Idara yake katika hafla fupi ya kumuaga baada ya kustaafu, Sherehe hiyo iliyofanyika katika Hoteli ya Simba Jijini Dodoma.*

# Malenga wetu

## KIBURI NYUMBA YA GIZA

1. Mwanadamu hasifiki, Ushupavu na Kiburi,
Kiburi huzaa chuki, majitapo si mazuri,
Ulimwengu hautaki, jambo lenye taksini,
Dawa Mirungi hatari, Wanajeshi tuyakane.

2. Si wajibu upasao,Vilema kuvikasiri,
Hujajua maishao, Viweje yatashamiri,
Anayedharau hayo, Mwisho wake hula mori,
Dawa Mirungi hatari, Wanajeshi tuyakane.

3. Moyo unahangaika, Sijui nifanye nini,
Kama ndege ningeruka,Kituo chngu Kambini,
Silaha ningejitwika, Kituo change Kambini,
Dawa Mirungi hatari, Wanajeshi tuyakane.

4. Mimi Siro namba wani, Kila ninapomuwazia,
Maisha kuyathamini, na mbinu zenye sheria,
Tumkabidhi manani, Juhudi nguvu na nia,
Dawa Mirungi hatari, Wanajeshi tuyakane.

5. Tumela Jeshi imara, limeweza kuzuwia,
Kwa vitendo na busara, Unyoofu na tabia,
Sio Jeshi la ujura, Litwishwe na kula dawa,
Dawa Mirungi hatari, Wanajeshi tuyakane.

6. Japo niko mbali nanyi, Kufika kila Kikosi,
Ninao wenge rafiki, Kwa maandiko nipateni,
Teja hasiwe Jeshini, Neleza wazi wazi,
Dawa Mirungi hatari, Wanajeshi tuyakane.

7. Makamanda ngazi zote, Seksheni kuanzia,
Hii vita yetu sote, Hadi ngazi ya Taifa,
Watenda tuwamulike, Biashara kukomesha,
Dawa Mirungi hatari, Wanajeshi tuyakane.

8. Nimelia vyakutosha, Nitoe mapendekezo,
Tuanze sema yatosha, Tena tuache mchezo,
Wengi waweza pisha, Tuzingatie vigezo,
Dawa Mirungi hatari, Wanajeshi tuyakane.

**Sgt Joseph Isaka Siro**
(Mshika Pembe Mkuu)
S.L.P. 928
**Pangawe, MOROGORO.**

## KILA LA KHERI KWANDIKWA

1. Ndimi sauti ya Lugha, naja kwenu wasifika,
Nikiwa nayo furaha, kusema ya kusikika,
Pasi kuwa na karaha, kunena ya kutukuka,
*Kila la kheri Kwandikwa, kwa yote unayotenda.*

2. Hakika nimeamua, kutoa yalo moyoni,
Yaweze kusisimua, kwa wote wanazuoni,
Nipate japo pumua, pamoja na ahueni,
*Kila la kheri Kwandikwa, kwa yote unayotenda.*

3. Ni mengi twajionea, tangu ushike kijiti,
Mazuri watutendea, ukiwa hapa ulinzi,
Mambo kadha yasogea, aliyoasisi Mwinyi,
*Kila la kheri Kwandikwa, kwa yote unayotenda.*

4. Ni mengi ya kukumbuka, aliyoyaacha Mwinyi,
Salama yaimarika, nayo mipaka ulinzi,
Wanajeshi kutosumbuka, maslahi wayaenzi,
*Kila la kheri Kwandikwa, kwa yote unayotenda.*

5. Mazoezi na mafunzo, hakika vyatekelezwa,
Nadharia kwa vitendo, pamoja vinafundishwa,
Shule pamoja na vyuo, navyo vinaimarishwa,
*Kila la kheri Kwandikwa, kwa yote unayotenda.*

6. Nayo malezi vijana, hakika hukuyasaza,
Jeshi Kujenga Taifa, malezi kuyasambaza,
Nayo mali kuzalisha, nao ulinzi Taifa,
*Kila la kheri Kwandikwa, kwa yote unayotenda.*

7. Mahusiano kujenga, mataifa duniani,
Amani inadumishwa, kwa nchi zisizo amani,
Askari Makamanda, kwa ustadi washiriki,
*Kila la kheri Kwandikwa, kwa yote unayotenda.*

7. Kuhawilisha tekno, watekelezwa kwa kina,
Nayo ya msingi mazao, kwa wingi yanazalishwa,
Kwa kuchangia mapato, mashirika yasimamia,
*Kila la kheri Kwandikwa, kwa yote unayotenda*.

9. Changamoto za bajeti, zote unazikabili,
Wazitatua kwa dhati, nasi pia twakubali,
Pasipo na kizingiti, tuweze kufika mbali,
*Kila la kheri Kwandikwa, kwa yote unayotenda.*

10. Nashusha yangu kalamu, niweze kupumzika,
Yabaki yalo muhimu, na yenye kuheshimika,
Nao muda umetimu, maneno kupunguzika,
*Kila la kheri Kwandikwa, kwa yote unayotenda.*

**Luteni Kanali Josephat M. Musira,**
(Sauti ya Lugha)
Sanduku la Posta 2924
**Dodoma**

# M&I JKT











**M&I JKT tunatoa huduma ya Chakula na Vinywaji katika Mikutano, Warsha, Semina na Sherehe mbalimbali Kama Kitchen Part, Send off na Harusi.**

**Tunapatikana Mgulani JKT, Wasiliana nasi kwa: 0716-226885**

**Pia tunatoa malazi katika hotel yetu ya Kisasa Mbweni JKT Club Wahi ujipatie huduma katika mandhari nzuri kwa bei nafuu**

**Kwa Mawasiliano Simu: 0715-303434**

# 'Katumieni Weledi mlioupata Chuoni' Waziri Kwandikwa

## ● Awaasa Wahitimu wa Ukamanda na Unadhimu-CSC

**Na Sajinitaji Subira Asukile**

Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga na Taifa Mhe. Elias John Kwandikwa (Mb) amewataka Maafisa wakuu wanaobahatika kupata Mafunzo ya Ukamanda na Unadhimu (CSC) Duluti, kutumia vizuri maarifa na ujuzi wanaoupata ili kuleta tija kiutendaji katika nyadhifa zao kijeshi.



Waziri Kwandikwa aliyasema hayo Juni 19, 2021 katika Mahafali ya Chuo hicho alipokuwa mgeni rasmi ambaye pamoja na mambo mengine alifunga mafunzo ya Ukamanda na Unadhimu Kundi 35/20 katika Chuo cha Ukamanda na Unadhimu (CSC) Duluti Jijin Arusha. Mafunzo yaliyodumu kwa muda wa mwaka mmoja.

"Maarifa na ujuzi wa Kijeshi unaotolewa hapa kwa Maafisa wakuu wa Jeshi, mara zote umekuwa ukileta tija katika utendaji kazi kwa nyadhifa wanazokwenda kuzitumikia, hasa kwa wakati huu wa mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa, kijamii na kijeshi, yanayoleta changamoto za Ulinzi na Usalama duniani,wanatakiwa pia kuendana na kasi ya mabadiliko hayo" Alisema Waziri Kwandikwa.

Waziri pia pongezi kwa Mkuu wa chuo hicho Brigedia Jenerali Silvester Ghuliku kwakufanikisha mafunzo hayo kwa maafisa Wakuu hao na pia akakipongeza Chuo cha Uhasibu Arusha kwa kushiriki katika kutoa mafunzo ya kimkakati ya Ukamanda na Unadhimu. Pia akawapongeza Wahitimu kwa kutimiza ndoto zao kumaliza na kufuzu mafunzo hayo.

Chuo cha Ukamanda cha Unadhimu tangu kuanzishwa kwake kililenga kutoa ujuzi na maarifa ya Kijeshi kwa majukumu ya ngazi za juu kwa Maafisa Wakuu huku kikilenga kuleta uwajibikaji makini, uamuzi sahihi na utatuzi wa migogoro bila kutumia nguvu, kuwa na mahusiano na ushirikiano mzuri Kimataifa.

"Mmepata ujuzi mkubwa na mahitajio mapya ya Kijeshi sambamba na maarifa vyote hivi vibaki katika fahamu na akili zenu kuwa ni mtaji wa uwajibikaji. Nendeni mkayatumie kwa faida ya nchi zenu" alitanabaisha Waziri Kwandikwa kwa wahitmu.

Kundi 35/20 limejumuisha wahitimu kutoka Nchi saba (7) ukianza na Tanzania wenyewe, Falme ya Eswatini, Burundi, Misri, Kenya, Malawi na Uganda.

Nchi za Afrika zimekuwa wadau wakubwa kwa kuleta Maafisa Wakuu wa Majeshi yao ili kupata mafunzo ya Kimkakati ya Ukamanda na Unadhimu, hii inatokana na Ubora wa mafunzo yanayotolewa na Chuo hiki nchini hapa

Chuo cha Ukamanda na Unadhimu (CSC) kilichopo Duluti Jijini Arusha, tangu kuanzishwa kwake mwaka 1979 miezi michache baada ya kumalizika kwa Vita ya Kagera, kimeendelea kuwa na rekodi nzuri na kubaki kuwa Kitovu cha Ujuzi na Maarifa ya Kijeshi Afrika Mashariki na Afrika nzima.



*Wakuu wa Bodi ya Chuo cha Ukamanda na Unadhimu siku ya Mahafali Chuoni hapo*

# Mjue Rais mwenye Umri Mdogo Duniani

- **Alikuwa Rais Akiwa na Umri wa Miaka 25**
- **Rekodi yake bado haijavunjwa**
- **Alikuwa Rais kati ya Mwaka 1992-1996**
- **Akiwa na Cheo cha Kapteni**



**Na Kapteni Mohamed Idd**

Valentine Melvine Strasser kwa jina maarufu alijulikana kama Valentine Strasser ni Rais ambaye aliwahi kutawala akiwa na umri wa miaka 25 nchini Sierra Leone. Valentine Strasser alizaliwa tarehe 26 Aprili, 1967 Mjini Freetown Nchini Sierra Leone, akitokea kwenye kabila Creole linalopatikana mashariki mwa mji mkuu wa Sierra Leone. Wakati strasser anazaliwa Sierra Leone ilikuwa nchi inayoongozwa kwa mvumo wa Serikali ya Kibunge.

Valentine Strasser alipata elimu katika shule za kidini za Kianglikana hadi kufikia mwaka 1985 alihitimu masomo ya Sekondari katika shule ya Grammar iliyopo Freetown akiwa na umri wa Miaka 18. Strasser wakati anahitimu Shule ya Sekondari alikuwa Mwanafunzi bora katika masomo ya Sayansi na Hesabati.

Wakati anamaliza masomo yake ya sekondari alipata bahati ya Kuandikishwa Jeshi la Ulinzi la Sierra Leone akiwa na Umri wa Miaka 19. Baada ya kuhitimu mafunzo ya awali ya kijeshi Valentine Strasser alipata tena nafasi ya kujiunga na mafunzo ya Uafisa mwanafunzi katika Chuo cha Maafisa wa Kijeshi Benguema nje kidogo mwa Mji wa Freetown.

Baada ya kuhitimu na kutunukiwa Kamisheni na Kuwa Afisa wa Jeshi, alipangiwa kufanya kazi katika kambi ya kijeshi ya Daru Wilayani Kailahun Mashariki mwa Sierra Leone. Mwaka 1992 Vuguvugu la Waasi lilianza kufanya mashambulizi yalioongozwa na Foday Sankoh na kikundi chake kilichojiita "Revolutionary United Front" (RUF) Wilayani Kailahun katika vijiji vya Buedu ambapo Kapteni Valentine Strasser alikokuwa akifanyia kazi. Strasser na Wanajeshi Wengine waliopo Wilayani Kailahun walianza kupambana na waasi wa RUF chini ya Kiongozi wao Foday Sankoh.

Wakati wa Vita Wilayani Kailahun, Serikali ya Sierra Leone iliyokuwa ikiongozwa na Rais Joseph Saidu Momoh walishindwa kutoa mahitaji muhimu kama vifaa na zana kwa ajili ya wanajeshi ambao wanapambana na kundi la waasi RUF chini ya Foday Sankoh. Serikali ya Sierra Leone walishindwa kuwalipa wanajeshi mishahara kwa wakati na kupelekea wanajeshi waliongozwa na kapteni Strasser kuandamana kuelekea mji Mkuu wa Freetown wakiwa wamevaa sare za kijeshi.

Waandamanaji walikuwa wanadai malipo ya malimbikizo ya Mishahara na kusahauliwa kwao wakati wapo uwanja wa vita dhidi ya RUF chini ya Foday Sankoh. Kundi hii lililongozwa na Strasser akiwa na Kapteni Sahr Sandy na Sajini Solomon Musa, maandamano ya askari katika mji wa Mkuu Freetown yalipelekea Rais Momoh kukimbilia uhamishoni katika mji wa Conakry nchini Guinea.

Hali hii ikapelekea Valentine Strasser kushika madaraka akiwa na Umri mdogo wa miaka 25 na kuwa Rais mdogo kuliko wote Duniani kwa Wakati huo, pia rekodi yake haijawahi kuvunjwa na kiongozi yeyote aliyewahi kushika madaraka akiwa chini ya Umri wa Valentine Strasser.

Strasser alikuwa kiongozi wa Serikali ya Mpito ya Kijeshi ya Sierra Leone kati ya mwaka 1992 hadi kufikia mwaka 1996 alipopinduliwa na washirika wake wa karibu wakiongozwa na Msaidizi wake Brigedia Jenerali Julius Maada Bio, kwa kushirikiana na Kanali Tom Nyuma, Kapteni Komba Mondeh ambao hawakufurahishwa na uongozi wake jinsi alivyoshughulikia masuala ya amani katika kurudisha utawala wa kiraia.

Januari 1996 Kapteni Valentine Strasser alipinduliwa katika mapinduzi ya kijeshi na kuwa mwisho wa Utawala wake. Strasser aliweza kuomba hifadhi kwa Umoja wa Mataifa uliompatia nafasi ya kipekee kwenda Nchini Uingereza kwenda kusoma shahada ya Sheria katika Chuo Kikuu cha Warwick Mjini Coverty. Kwa Bahati Mbaya Strasser aliweza kusoma kwa miezi 18 na kushindwa kulipia gharama za masomo.

Valentine Strasser aliamua kurudi kwao Nchini Sierra Leone katika kijiji alichozaliwa. Serikali ya Sierra Leone kwa wakati huo haikumpa mahitajio na huduma kama Rais Mstaafu, Kapteni Strasser aliishi kwa shida na dhihaka nyingi kutoka kwa watu mbalimbali na wengine walimuita Rais maskini kuliko wote Duniani.

Kwa Bahati nzuri waswahili wanasema kabla ya hujafa haujaumbia Strasser ameishi kwa shida lakini baada ya dhiki ni faraja. Rafiki yake Brigedia Jenerali Julius Maada Bio aliyempindua mwaka1996 naye hakudumu katika nafasi hiyo aliyodumu kwa takriban miezi miwili kuanzia Januari 16, 1996 hadi Machi 29, 1996 naye akapinduliwa. Mabadiliko ya kisiasa yakafanyika nchini Sierra Leone na kupelekea Uchanguzi huru wa Mwaka 2018 wa vyama vingi vya kisiasa na kupelekea Brigedia Julius Maada Bio kuwa Rais kutoka kwenye muunganiko wa vyama vya Upinzani.

Rais Maada Bio wakati wa kampeni za Uchaguzi wa Mwaka 2018 moja ya ahadi yake kwa wananchi wa Sierra Leone ni kumuangalia tena Kapteni Strasser kwani alikuwa kiongozi mzalendo na mpenda nchi yake kwa kupigania amani wakati wa Vuguvugu la Uasi wa Mwaka 1992.

Kwasasa Kapteni Valentine Strasser anapatiwa staihi zote kama kiongozi mstaafu wa Sierra Leone, Rais Maada Bio ameweza kumjengea makazi ya kudumu nje kidogo na mji mkuu wa Sierra Leone. Rais Maada Bio hakuishi hapo kumsaidi rafiki yake ambaye walipigana na Waasi wa RUF kwa matibabu ya Mguu ambao aliyeruhiwa wakati wa mapambano. Valentine Strasser amefanyiwa matibabu ya mguu wa kushoto ambao umepelekea kukatwa na kwa sasa Kapteni Strasser amebakia na mguu mmoja wa kulia.

# Misingi ya Upigaji Picha na Matumizi yake

**Na Luteni Kanali Josephat Musira**

Upigaji picha ni njia mojawapo ya mwasiliano katika maisha ya kila siku ya mwanadamu. Mawasiliano kwa njia ya picha yameanza kutumika tangu miaka 1840 baada ya kuvumbuliwa kwa kamera. Matumizi ya njia hii ya kupashana habari imeshika kasi kwa siku za karibuni kwa kuwa ni njia rahisi na ya haraka kwa watumiaji kwa wale wanaojua kusoma na kuandika na hata kwa wale wasiojua kusoma wala kuandika. Kwa kufanya hivyo wanataka hata kuwapiku waliosomea taaluma ya habari hususan wapigapicha.

Mpigapicha anaporipoti habari yake kupitia picha ama anaripoti uhalisia wa tukio lenyewe kwa njia ya picha. Na picha nzuri ni ile ambayo inaripoti maisha ya mwanadamu vizuri zaidi kuliko kuongea ama kuandika.

Picha inao uwezo wa kufafanua tukio ikiwa ni pamoja na kuonyesha uhalisia (mood). Tofauti na mandishi yanayotumika kufafanua au kusistiza jambo ambapo msomaji anaweza kuchukua muda mrefu kidogo kuvuta hisia za kile kilichoaandikwa ili aweze kumwelewa mwandishi kuhusu tukio husika. Lakini matumizi ya picha yanashawishi na kuvutia maana picha moja inao uwezo wa kuongea maneno zaidi ya elfu moja kwa wakati mmoja.

Katika kuandika habari za picha ama matukio katika picha ni sharti mpigapicha awe na uwezo pamoja na uelewa katika kukusanya na kuandika habari hiyo kwa njia ya picha. Aidha, habari katika picha ni lazima izingatie 5W+H; Nani amehusika katika tukio?; Wapi tukio limetokea?; Kwa nini limetokea?; Nini kimetokea?; Lini tukio limetokea?; na kwa namna gani tukio hilo limetokea?

Mpigapicha mzuri ni yule anayezingatia matumizi mazuri ya kamera na namna inavyofanya kazi kwa kuzingatia *'rule of third'*. Kutokana na kukua kwa sayansi na teknolojia pamoja na kushamiri kwa matumizi makubwa ya simu za mkononi zenye uwezo wa kupiga, kuhifadhi na kutuma picha (*smartphones*).

Hivi sasa kila mtu anaweza kujiita mpigapicha pasipo kuzingatia maadili, kanuni, misingi na taratibu za upigaji pamoja na matumizi ya picha. Mfano ni upigaji picha majeruhi wa ajali, mtu anakula, n.k. na kuzirusha kwa mtu mwingine ama makundi ya WhatsApp, Tovuti, mitandao ya kijamii, n.k. kwa lengo la kutoa taarifa, kuelimisha, kuburudisha, kukosoa, na kadhalika.

Mpigapicha anatakiwa kuzingatia maadili ya kazi yake kwa kuwasilisha uhalisia wa tukio ili aweze kujenga mahusiano mazuri na jamii inayomzunguka kwani watu wanaamini kuwa kamera haiwezi kuongopa. Hata kama ataichezea picha lazima watu wataamini kuwa kuwa picha iko sahihi, japo siku hizi kuna baadhi ya watu wanaweza kutofautisha picha halisi na isiyo halisi.

Picha zinazopigwa hazina budi kuangukia katika makundi haya picha za kihabari; picha za kimakala; picha za … na matukio katika picha.




*Mpiga picha wa Gazeti la The Guardian Tanzania Bi. Halima Kambi akionesha umahiri wake katika Upigaji picha*

# Waziri Mkuu Aitaka NDC kujiwekea Malengo endelevu

## • Ni katika Mahafali ya Tisa Chuo cha Taifa cha Ulinzi

**Na Sajini Lazarus Masanja**

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa ameutaka uongozi wa Chuo cha Taifa cha Ulinzi (NDC) kujiwekea malengo endelevu yatakayokifanya kiwe Chuo bora chenye kutegemewa na Taifa katika masuala ya Ulinzi kwa ujumla katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Waziri Mkuu aliyasema hayo Julai 22,2021 katika Mahafali ya tisa ya Chuo cha Taifa cha Ulinzi kilichopo Kunduchi nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam ambapo kozi ya masuala ya Ulinzi, Usalama na Mikakati ilihitimu mafunzo hayo.

Alisema Serikali itahakikisha kuwa Chuo hicho kinakuwa ni kituo cha ufahari katika kutoa elimu ya juu kwa maafisa watendaji kutoka katika vyombo vya Ulinzi na Usalama na Watumishi wa Umma.

"Serikali inatambua mchango wa Chuo hiki katika kutoa mafunzo yanayowajengea uwezo Viongozi na Watendaji mbalimbali kwenye masuala ya usalama na mikakati" Alisema Waziri Mkuu.

Alisema, mpaka sasa maafisa Wandamizi 300 kutoka katika Vyombo vya Ulinzi na Usalama ndani na nje ya nchi na wengine kutoka katika Taasisi za umma za kiraia wamenufaika na mafunzo haya yanayotolewa nan a Chuo hiki.

Waziri Mkuu pia amekitaka Chuo hiki kuhakikisha kinatoa mafunzo na utaalamu ambao utasaidia katika kukabiliana na matishio ya kiusalama ya karne ya 21 sambamba na vitendo vya ugaidi, usafirishaji haramu wa binadamu, madawa ya kulevya, janga la ugonjwa wa UVIKO-19 na uhalifu wa kimtandao.

Alisema Chuo hiki kimeendelea kuwa miongoni mwa sehemu muhimu katika ujenzi na uimarishaji mahusiano ya mtu mmoja mmoja kwa Washirika wa mafunzo yake sambamba kuimarisha mahusiano ya kimataifa kwa maslahi mapana ya nchi yetu Akizishukuru nchi washiriki Waziri Mkuu alezitaka nchi hizo kuendelea kukiunga mkono chuo cha NDC kwa kuendelea kuleta maafisa wao wandamizi ili wapate mafunzo.

Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Ulinzi Meja Jenerali Michael Muhona aliwapongeza wahitimu woote kwa kukamilisha mafunzo yao kwa weledi mkubwa na akatumia wasaa huo kuwapongeza kwa nidhamu nzuri waliyoonesha kwa kipindi chote cha mafunzo walipokuwa Chuoni hapo.

Jumla ya nchi saba zimeleta Maafisa wao wandamizi katika Program hii ya mafunzo yaliyohitimishwa leo, nchi hizi ni Bangladesh, Burundi, Kenya, Nigeria, Malawi, Uganda na Zambia.

Awali akimkaribisha Waziri Mkuu ili awahutubie wahitimu wa kozi hiyo ya mwaka mmoja Kansela wa Chuo hicho Balozi Dkt. Martin Lumbanga alisema kuwa wataendelea kusimamia ubora wa masomo yanayotolewa na chuo hicho ili kukifanya kiendelee kuwa na hadhi ya kimataifa katika utoaji wa elimu bora. Hii ni mahafali ya 9 tangu Chuo hiki kianzishwe.



*Sehemu ya Wahitimu wa Chuo Cha Ukamanda na Unadhimu wakiwa wamesimama wakati Wimbo wa Taifa ukipigwa ambapo Mgeni Rasmi alikuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassimu Majaliwa Kassim*




# SMH
## LOGISTICS COACH
**Furahia Safari na Usafiri Salama**

**DAR-DODOMA**
**DODOMA-DAR**
**KILA SIKU!**



**GHARAMA ZAKE NI NAFUU.**

### HUDUMA ZILIZOPO:
- Vinywaji na Vitafunwa.
- Viti Vya Starehe.
- Huduma ya Mtandao Bure.
- Runinga Za Kisasa.
- Kiyoyozi.
- Wahudumu nadhifu. Waliobobea Katika Kujali Mteja Kwa Viwango Vya Hali Ya Juu.
- Uhakika Wa Ulinzi na Usalama Kwa Abiria Na Mizigo yako.




### WASILIANA NASI:
0713 46262
0789 021042
E-mail smhlogisticscoach@gmail.com
www.smhlogisticscoach.co.tz

